

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



NA. 28 YA 1980

NAKUBALI,

Julius K. Nyerere
Rais

30 JULAI, 1980

Sheria ya kubadilisha baadhi ya Masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977, kwa madhumuni ya kubadilisha idadi ya Wabunge wanaowakilisha wilaya za uchaguzi ili idadi mpya ya Wabunge iwe sawa na idadi mpya ya wilaya za uchaguzi

[1 AGOSTI, 1980]

SHERIA hii imetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

KWA KUWA aya ya (b) ya ibara ndogo ya (1) ya ibara ya 23 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977, inaweka masharti kwamba idadi ya Wabunge wanaowakilisha wilaya za uchaguzi itakuwa ni mia moja na sita:

NA KWA KUWA wilaya mpya tano, ambazo ni wilaya za uchaguzi, zimezinduliwa, yaani, Wilaya ya Bunda, Wilaya ya Makete, Wilaya ya Mwanza, Wilaya ya Nkansi na Wilaya ya Ngorongoro:

NA KWA KUWA masharti ya aya ya (a) ya ibara ndogo ya (3) ya ibara ya 23 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977, yametoa kwa Bunge uwezo wa kutunga sheria kwa ajili ya kubadilisha idadi ya Wabunge wanaowakilisha wilaya za uchaguzi ili idadi mpya ya Wabunge iwe sawa na idadi mpya ya wilaya za uchaguzi:

KWA HIVYO, BASI, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linatunga Sheria ifuatayo:—

1. Sheria hii iitwe Sheria ya Mabadiliko ya Tatu katika Katiba ya Nchi, ya mwaka 1980, na itanza kutumika tarehe 1 Agosti, 1980.

Jina la
Sheria na
tarehe ya
kuanza
kutumika


Mabadiliko
katika
Katiba

2. Masharti ya aya ya (b) ya ibara ndogo ya (1) ya ibara ya 23 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977, yanabadilishwa kwa namna iliyoelezwa katika ibara ya 3 ya Sheria hii.

Kuongeza
idadi ya
Wabunge
wa
wilaya za
uchaguzi

3. Idadi ya Wabunge wanaowakilisha wilaya za uchaguzi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaongezwa kutoka mia moja na sita na kuwa mia moja na kumi na moja; na aya ya (b) ya ibara ndogo ya (1) ya ibara ya 23 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977, inabadilishwa kwa kufuta maneno "mia moja na sita" na kuwaka badala yake maneno "mia moja na kumi na moja".

Nathibitisha kuwa Muswada kwa ajili ya Sheria hii umepitishwa na Bunge kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 52 (1) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.


A. S. MKWAWA,
Spika

Imepitishwa katika Bunge tarehe 23 Julai, 1980.


E. E. KAZIMOTO,
Katibu wa Bunge